

Manyezi ya Utumwa katika Makutano ya Utumwa na Ukoloni na Athari yake katika Usemi wa Kitamaduni na Mtazamo wa Jamii za Afrika Mashariki

Ali H. Chembea¹

Ikisiri

Utumwa ni suala linalozua si tu manyezi katika fasihi ya Kiswahili bali pia linaakisi utata wa kihistoria na kijamii katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Fasihi ya Kiswahili imekuwa chemchemi yenye nguvu kueleza sauti za waliotengwa, kutambua hali halisi ya maisha ya utumwa, upinzani na ustahimilivu. Uchunguzi huu umeshughulikia makutano ya ukoloni na utumwa, ukionesha jinsi nguvu hizi zinavyoingiliana kuathiri usemi wa kitamaduni na mitazamo ya jamii. Kupitia diwani ya *Sauti ya Dhiki* iliyoandikwa na Abdilatif Abdalla na riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* iliyoandikwa na Adam Shafi ndani ya mifumo mipana ya kihistoria, waandishi wameonesha mateso ya kihisia-moyo na ya kimwili ya watumwa, hasa katika kuangazia mapambano yao ya kupata uhuru na utu. Makala hii inachanganua umuhimu wa kuelewa utumwa si tu kama ukweli wa kihistoria bali kama masimulizi yenye nguvu ambayo yanaendelea kuvuma katika matini za fasihi ya Kiswahili. Hatimaye, uchunguzi huu umesawiri ufahamu wa kina wa athari za utumwa, ukiangazia jukumu lake katika kujenga utambulisho wa kitamaduni na kukuza diskozi za kijamii katika mapambano yanayoendelea ya haki na utu.

1.0 Utangulizi

Utumwa ni mojawapo ya masuala nyeti na yenye uzito mkubwa katika fasihi ya Kiswahili kwa kuwa unaakisi maumivu, mapambano na matumaini katika jamii za Afrika Mashariki. Baadhi ya watu wamekuwa wakipata kigugumizi kuzungumzia au kujinasabisha na historia hii dhalimu. Katika makala hii, nakutanisha mifumo miwili ya kiuchumi iliyolazimishwa katika bara la Afrika, hususan katika Ukanda wa Afrika Mashariki ambapo ushahidi unathibitisha kuwa madhila ya utumwa visiwani Zanzibar na Kenya yalikuwa bayana katika unyonyaji wa nguvukazi na kuongezeka kwa matabaka. Utumwa ulitumika kama nyenzo ya kuwazalishia mali wenye nguvu kwa kuwatumia wanyonge wasio na nguvu bila hiari yao. Ukoloni ulikuja baada ya mapinduzi ya viwanda huko Ulaya mwishoni mwa karne ya 18 na mwanzoni mwa karne ya 19 na mabepari wa dola kubwa za Kimagharibi walifanya

¹ Mhadhiri, Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu, Chuo Kikuu cha Pwani, Kenya.
Baruapepe: alichemtsy@yahoo.com

kila lililowezekana mkunyang'anya malighafi na nguvukazi za bara la Afrika kukidhi uhitaji mkubwa wa rasilimali ulioibuka kufuatia maendeleo ya viwanda.

Makala hii inakutanisha utumwa na ukoloni kwa kuonesha namna vilivyowakandamiza raia kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mifumo hii, kando na tofauti zake kiasili, ni sera moja ya kiuchumi ya wenye nguvu kuwanyonya wanyonge, hasa mabepari waliojiweka tabaka la juu kwa rangi, mamlaka au mali dhidi ya tabaka la chini, yaani wasionavyo. Katika utumwa na umwinyi, wanyonge walikuwa vijakazi au watwana na mali ya kutumiwa na mabwana zao kama watakavyo; wa kuuzwa wakauzwa na wa kutumikishwa wakatumiwa. Mamwinyi wenye mashamba makubwa-makubwa walimiliki watumwa wa kununuliwa au wa kutumikishwa bila huruma kwa ajira ya kijungu-jiko. Katika kipindi hiki, wakoloni walikuja na wakatagusana na utumwa na umwinyi kwa upande mmoja na ukoloni na ubepari kwa upande mwingine. Utumwa na umwinyi ukawa nguzo ya kukita ukoloni. Pindi utumwa ulipokomeshwa nchini Kenya kupitia sheria ya mwaka 1905 na Tanganyika kupitia sheria ya mwaka 1922, ukapisha ukoloni ambao uliendeleza utumwa kwa njia nyingine ikiwa ni pamoja na mfumo wa manamba. Ingawa kwa sasa utumwa na ukoloni havipo kwa sura zake za asili, fasihi ya Kiswahili haikusahau athari zake katika historia ya jamii za Afrika Mashariki.

2.0 Utumwa katika Jamii za Afrika Mashariki

Utumwa umekuwapo katika jamii za Afrika Mashariki, ukiathiri nyanja muhimu za maisha kama vile uchumi, siasa na utamaduni. Jamii mbalimbali zilishiriki katika utumwa kama wajakazi, wamiliki na wafanyabiashara. Baadhi ya jamii za Kiafrika zilikuwa na utumwa wa kijadi ulioibuliwa na vita, madeni au makosa ya jinai. Kwa mujibu wa Kimambo na Temu (1969), jamii nyingi za Kibantu zilikuwa na watumwa waliotumika kama wafanyakazi wa nyumbani au wa shambani na wakati mwingine waliolewa na kuunganishwa katika familia za wamiliki wao.

Ujio wa Waarabu kuanzia karne ya 18 hadi 19 ulipanua mfumo huu katika kiwango cha biashara ya kimataifa. Waarabu walihusisha pwani ya Afrika Mashariki, hasa Zanzibar, Bagamoyo, Kilwa na Pemba, katika mtandao mkubwa wa biashara ya watumwa na pembe za ndovu. Kwa mujibu wa Allen (2014), biashara hii ilihusisha maelfu ya watumwa waliochukuliwa kutoka maeneo ya bara kama Nyasa, Tabora na Tanganyika ya Kati na kuuzwa katika masoko ya pwani au kupelekwa Mashariki ya Kati na Asia. Watumwa hawa walitumiwa kulima mashamba ya karafuu, kufanya kazi za nyumbani au kutumika kama bidhaa ya kibiashara.

Kulingana na Illife (1979), mtazamo wa biashara ya watumwa ulibadilika mara baada ya ujio wa wamisionari na wakoloni kutoka Ulaya hasa David Livingstone waliopinga vikali biashara hii kwa madai kuwa ni kinyume na maadili na mafundisho ya Kikristo. Hata hivyo, Sheriff (1987) anadai kuwa upinzani wa Ulaya haukuwa kwa misingi ya kidini au kibinadamu bali propaganda za kisiasa na kiuchumi kwani walitaka kudhibiti njia za kibiashara na ushawishi wao katika kanda

ya Afrika Mashariki. Hivyo, kupitia miktaba ya kibiashara kama ule wa 1873 kati ya Sultan wa Zanzibar na Waingereza, biashara ya watumwa ilianza kupungua rasmi japo ilidumu kwa siri hadi mwanzoni mwa karne ya 20.

Utumwa hauhusu tu kuuzwa na kununuliwa kwa watu bali kulazimishwa jambo usiloridhia. Si tu kinyume cha uungwana (Eastman, 1994), bali utumwa upo wa kulazimishwa kufanya kazi bila malipo na utumwa wa kutumikishwa kinyume na haki ili kupata riziki (Mwathi na wenzake, 2024). Odetola na Ademola (1987) wanasema kwamba utumwa haupo lakini umwinyi unadhihirika pale ambapo wasio na ardhi hutegemea wenye ardhi kwa kuuza nguvukazi zao kwao au kukodi ardhi zao ili wapate riziki. Aidha, utumwa umekuwa nyenzo ya mataifa makubwa ya Kimagharibi kuzalisha mali kwa kuyatawala kimabavu mataifa ya Afrika. Kuptia ukoloni, mataifa ya Kimagharibi yalipata haki ya kumiliki chochote yalichoona kina manufaa kwao dhidi ya Mwafrika mwenyewe. Sharma na Gupta (2015) wanausawiri ukoloni kama uvamizi wa rasilimali za kiasili za mataifa machanga na mataifa ya Kimagharibi. Ukoloni na ubepari ulikuwa sehemu ya msukumo wa nguvu iliyoendeleza biashara ya watumwa (Givens, 2022). Kimsingi utumwa uliwaona Waafrika kama watu-nusu ilhali ukoloni uliwaona kama washenzi ambao walihitaji kufunzwa ustaraabu (Givens, 2022).

Kuzuka kwa wenyenavyo na wasionavyo ndio utabaka kwani kimsingi umekita kwenye uwezo wa kiuchumi. Tabaka la wenyenavyo huwa juu ya tabaka la wasionavyo ambao ni watu walio chini. Kuwapo kwa matabaka haya mawili katika jamii husababisha kuzuka kwa mivutano baina ya makundi haya mawili. Tabaka la juu linataka kutumia jasho la walio chini kulimbikiza mali na rasilimali zaidi huku tabaka la chini likipigania haki ya kutonyanyaswa na ugavi sawa wa nyenzo za kiuchumi na umiliki wa njia kuu za uzalishajimali. Kuchuma kukawa ubepari wa mwenye nguvu mpishe ambapo watu wachache walimiliki mali na nyenzo kuu za kiuchumi na umati wa wengi ukatopea kwenye unyonge, udhalili na umaskini. Wanyonge, ambao ni Waafrika, wakiwa katika hali ya kujikunakuna kwa machungu walipata ari ya kufurukuta kutafuta ukombozi.

3.0 Diwani ya Sauti ya Dhiki na Riwaya ya Kasri ya Mwinyi Fuad

Diwani ya *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973) ilitungwa na Abdilatif Abdalla baada ya ukoloni mkongwe kupisha nafasi ukoloni mamboleo nchini Kenya. Ni kilio cha sauti ya wanyonge wanyongwao akiwemo mshairi mwenyewe kutokana na ukatili wa ukoloni katika sura zake mbalimbali. Abdalla aliandika diwani hii wakati alipokuwa akitumikia kifungo cha miaka mitatu katika gereza la Shimo la Tewa kwa sababu alipatikana na hatia ya kuchochea watu kupindua serikali ya Kenya kwa kutumia "silaha" baada ya kuandika makala aliyoiita "Kenya Twendapi?" (Kresse, 2016). *Sauti ya Dhiki* ni kumbukumbu muhimu ya kihistoria kuhusu matukio ya kipindi hicho katika uchanga wa taifa la Kenya. Mshairi anaazimia kutafuta haki na kuhakikisha kuwa sauti kwa waliodhulumiwa katika jamii inakuwa thabiti. Abdalla anaeleza kuwa mashairi yote yaliyomo kwenye *Sauti ya Dhiki* aliyatunga kifungoni

isipokuwa “N'sharudi” (uk. 123) alilolitunga baada ya kutoka jela. Anwani ya “Sauti ya Dhiki” ni ishara ya maisha ya mateso wanayopitia wanyonge katika jamii.

Riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* (Shafi, 1978) iliandikwa na Adam Shafi baada ya umwinyi uliokitwa ukoloni mkongwe na kupisha ukoloni mamboleo visiwani Zanzibar. Ni taswira ya juhudi za wanyonge kupindua umwinyi uliowatumikisha na kukaribisha uhuru. Shafi aliandika kusawiri mvutano baina ya ubwana kwa upande mmoja na unyonge kwa upande mwingine. Ni katika kipindi cha baada ya kutumikia kifungo cha miaka miwili kufuatia tuhuma zilifungamana na mauaji ya aliyekuwa mwanzilishi wa Jamhuri ya watu wa Zanzibar, Abeid Karume (Vierke, 2024). Mabwana wenye kumiliki mashamba makubwa wanaishi maisha ya starehe ilhali watumishi wao wanaishi maisha ya kukatisha tamaa. *Kasri ya Mwinyi Fuad* ni hazina kuu ya kihistoria yenye kutoa kumbukizi za hatima ya udhalimu na matumaini kwa wanyonge kuushinda ubepari pindi wanapopigania haki na utawala bora. Shafi anaonesha wajibu wa kusimama imara kuung'oa utawala usiozingatia haki kwa nguvu wala si vinginevyo kwani hautang'oka pasi na mkakati wa kimakusudi unaohusisha kuhatarisha maisha.

3.1 Taswira za Ukoloni na Ukoloni Mamboleo katika *Sauti ya Dhiki*

Ukoloni wa Mwingereza kabla ya kupisha ukoloni mamboleo ulitawaliwa na mabavu na ukatili. Mathalani, mshairi Abdalla akitumia jazanda ya wanyama wa mwituni katika shairi la “Mamaetu Afrika” anaonesha jinsi mkoloni alivyomsawiri Mwafrika kama mnyama asiyestahiki ubinadamu bali unyama : *si watu hawa, ni wanyama wa mwituni*. Hivyo, akajipa kibali cha kuwakandamiza wenyeji kwa kunyakua ardhi na rasilimali zake. Mshairi anasema : *Mali nyingi ya thamani, wakakupokonya Mama*. Wakazidisha kejeli kwa kuwaita manyani kwa kuwa weusi, yaani viumbe wasio na hadhi ya binadamu—watu washenzi—wasiostahiki ustaarabu au kustahiki chochote. Anasema katika *ubeti* wa saba :

*Hawakuthamini utu, wa walo na ngozi hini.
Wakituona manyani, kwamba tu weusi Mama.*

Mkoloni pamoja na nguvu na mamlaka aliyokuwa nayo, alihofia umoja wa Waafrika, hivyo, akapanga mkakati wa kuwatenganisha ; yaani tenga-tawala ili kuwapiganisha wao wenyewe kwa wenyewe. Mshairi anasimulia tukio hilo la kuhuzunisha katika ubeti wa kumi na tano:

*Hapa wakakatikiwa, kwamba watutenganishe
Kwani wamoja tukiwa, tutawakanyanga weshe
Wakaona kubwa dawa, wano watutenganishe
Ili wakukorofishe, na kukunyonya we Mama*

Hatua hii ilisababisha umwagikaji mkubwa wa damu wakati Maumau walipovamia na kuua ndugu zao waliosemekana wanashirikiana na wakoloni; na hatimaye, mauaji makubwa ya Wakenya yakatokea. Katika ubeti wa ishirini na moja mshairi anasema:

*Nyingi mno damu yetu, ikabidi kumwaika
Baadhi ya ndugu zetu, roho zao zikatoka
Na kila kilicho chetu, kwa wingi kikatumba
Kwa kutaka kuiweka, hadhi yetu nawe Mama*

Baada ya juhudi za ushirikiano wa kuung'oa ukoloni, mkoloni alihujuru lakini hakuondoka patupu; alirudi kwa mlango wa nyuma akapisha ukoloni mamboleo. Katika shairi "Telezi" mshairi ameonesha ukatili wa ukoloni mamboleo ulioendeleza sera ya mkoloni kwa ukandamizaji, vitisho na kwa mauaji. Utawala wa raisi aliyechukua hatamu za uongozi baada ya mkoloni kung'oka haukutaka kukosolewa au kupata upinzani wa aina yoyote. Kwa kutumia jazanda ya wakulima (wananchi) waliopitia kazi ngumu (juhudi za kupigania uhuru) kupanda mimea (kuteua viongozi) hawakuvuna matunda yoyote, yaani matarajio waliyokuwa nayo baada ya mkoloni kuondoka hayakuonekana bali walibaki katika dhiki zao. Katika ubeti wa pili anasema:

*Mimeya walioipanda, ilitekukatekuka
Kazi ngumu walotenda, yote ikiharibika
Hawakuvuna matunda, waliyo wakiyataka
Waliyo wakiyataka, yakawa ya mbali nao*

Katika ubeti wa sita, mshairi anaonesha yaliyomfika pale alipotiwa jela (*kuendeya ndoana*) kwa kuandika karatasi ya "Kenya Twendapi?" iliyokuwa ikikosoa utawala uliokuwapo. Mwendo wake huo wa kusema waziwazi (*kwenenda japo kwa dhiki*) ukamponza.

*Japo hivyo zilikuwa, ndiya hazipitiki
Bali mimi haamuwa, kwenenda japo kwa dhiki
Kumbe vile nitakuwa, ni mfano wa samaki
Ni mfano wa samaki, kuiendeya ndoana*

Ilimbidi Abdalla abadilishe mbinu ya ukosoaji alipotiwa kizuizini. Katika ubeti wa saba anaeleza kuwa alijifunza mbinu mbadala ya kukosoa asije akaingia matatani. La muhimu kwa mshairi kama sauti ya jamii, ni kuendelea na utamaduni wake, Yaani kusema jinsi ukweli ulivyo kuhusu utawala uliopo, si kunyamaza kama inavyotaka serikali wakati makosa yanapofanyika katika uongozi. Mtazamo wake

wa kutaka nchi iwe mahali pema penye manufaa kwa wote haukutetereka licha ya kutiwa kifungoni. Tija yake ya kubadilisha mwendo wa kutembea (kukosoa) ikawa lugha fiche ya ushairi wa *Sauti ya Dhiki*. Anasema:

*Zikanibwaga telezi, sikujuwa kuzendeya
Ningekwenda kwa henezi, yazingenifika haya
Lakini tena siwezi, mwendo huo kutumiya
Sitawata kutembeya, ila tabadili mwendo*

Utamaduni huu wa kusema haki hata kama atafikwa na mawi kwa kuwa haikubaliki kwa viongozi tawala, ndio unaokaririka katika mashairi yake “N’shishiyelo ni lilo” na “Siwati” na kubaki na mtazamo wake wa kutaka viongozi wawajibikie majukumu yao. Katika “N’shishiyelo ni lilo” ubeti wa kumi na sita mshairi anasema kuwa hata akiteswa hataacha kusema.

*Mateso yao yangawa, nda kuumiza mtima
Hayatakuwa ni dawa, ya kutonipa kusema*

Vivyo hivyo, katika shairi la “Siwati” mshairi anasema kuwa hawezi kuacha mtazamo na msimamo wake wa kutaka uongozi mwema unaojali masilahi ya raia. Hilo kamwe hawezi kwenda kombo nalo hata kama atafikwa na madhila au kuambiwa kwamba hayo hayawezi kuwa na kwamba aridhie hali ilivyo. Mshairi anasema hatabadili mtazamo wake. Katika ubeti wa nne anaeleza:

*Siwati nimeradhiwa, kufikwa na kila mawi
Siwati ningaambiwa, niaminiyo hayawi
Siwati kisha nikawa, kama nzi, hivyo siwi
Thamma nakariri siwi, na M’ngu nisaidiya*

Hali hiyo ya ukoloni mamboleo ndiyo inayojitokeza katika mashairi mengine kama vile, “Mamba”, “Mnazi: Vute N’kuvute”, “Ah! Mwenzangu”, “Mja si Mwema”, “Usiniuwe”, “Sikakanawe na Kimya”, “Kutendana”, “Mwerevu Hajinyowi” na mengineyo. Ujumbe unaojitokeza katika mashairi haya ni ule wa kusuta viongozi waliojitwika majukumu ya kuiongoza jamii, kugeuka na kuwa nduli wanaohujumu jamii yao. Wamejivika kiburi na ubepari wa kuifakamia rasilimali ya nchi ambayo kimsingi inafaa kutumika kwa manufaa ya wananchi wote.

Katika shairi “Mnazi : Vuta N’kuvute”, kwa mfano, mshairi anasema :

Alii

-
7. *Mnazi ni wa shirika, mimi na wewe mwendani
Unshakuwa wataka, kunitowa shirikani ?
Hilo halitatendeka, wala haliwezekani
Sikubali abadani*
9. *Mnazi yake aswili, uli mbwa wazazi wetu
Mbwa baba zetu wawili, pasi wa kungiya wa tatu
Mali yao ya halali hawakunyang’anya mtu
Sasa wafile ni wetu*

Badi

24. *Wanambiya nilikuwa, nilikuwa, kilo kichache hikupa
Nami kingi hitukuwa, wanangu henda ’henda kuwapa
Ndiyo sababu wakawa, wanangu wamenenepa
Na nguo njema kuwapa*
-

Katika beti hizi, mshairi amemchora mhusika Alii anayewakilisha wananchi ambao wanalalamika kwa ndugu yao Badi aliyechukua hatamu za uongozi kwa ulafi na ubinafsi mkubwa akijilimbikizia kila aina ya mali kwa fujo bila kujali ndugu walioshirikiana kumwondoa mkoloni ili mnazi (rasilimali zao) wafaidi wote. Hataki kusikia wala kuambiwa bali ametawaliwa na kiburi kana kwamba ataishi milele. Mshairi anamkejeli kiongozi huyo jabari katika shairi “Mamba” ili angaa azindikane. Anasema katika ubeti wa pili:

*Kuna mamba, mtoni metakabari
Ajigamba, na kujiona hodari
Yuwaamba, kwamba ’taishi dahari*

Katika ubeti wa mwisho, mshairi anampa indhari kwamba kuna siku atakoma kuishi kama hatapatikana wa kumwondoa uongozini; hata awe na nguvu au kutumia vitisho vya kiasi gani, hawezi kushinda kifo. Utamaduni wa jamii haumruhusu mtu kunyamazia maovu bali unamtaka ayakanye kwa upeo wa uwezo wake japo viongozi wabaya hawakubali. Hili linamfanya mshairi asikome kumkosoa kiongozi ambaye kwa nguvu alizohodhi si rahisi kwamba atapatikana atakayeweza kumwondoa. Pamoja na uhalisia wa hali hiyo, mshairi habadili mtazamo wake kwamba uovu una mwisho na kwamba kuna siku uongozi wake utakoma kutokana na nguvu za maumbile.

*Afhamu, mtu hajui la kesho
Hatadumu, angatumiya vitisho*

Maadamu, lenye mwanzo lina mwisho

Kauli hiyo ya kuonya ya mshairi ipo pia katika shairi la “Mwerevu Hajinyowi” pale mshairi anaposema katika ubeti wa nne kuwa:

*Kupata kusikughururi, ukajidhani mwerevu
Na hicho chako kiburi, ujuwe ni maangavu
Iko siku itajiri, ujikute mwenye wavu
Tangu lini mwerevu, akajijowa mwenyewe?*

Kiongozi anaonywa asidanganyike akawa na kiburi kwa nguvu na mamlaka aliyonayo kwani vyote hivyo vina mwisho wake. Pia, pindi hatima itakapobisha, hapatakuwa na ujanja wa kujinasua au kumnusuru.

3.2 Taswira ya Utumwa na Ukoloni katika *Kasri ya Mwinyi Fuad*.

Umwinyi uliokitwa kwenye ukoloni wa Mwingereza ulimiliki watu, ukakandamiza na kutumikisha Waafrika; afadhali mnyama alipata haki ya kulishwa na kutunzwa. Kwa mfano, inaelezwa kwamba wazazi wa Kijakazi walikuwa miongoni mwa watumwa watiifu wa Bwana Malik, hawakuwa waungwana au watu huru bali walimilikiwa na bwana wao. Bwana Malik alikuwa kati ya mamwinyi waliomiliki mashamba makubwa na watumwa wa kutumikishwa. Utiifu wa wazazi wa Kijakazi haukuwa kasoro kwao kwa kuikubali hali yao ya utumwa kama kawaida ya maisha kwao. Huo ukajenga mwendo wao kinyume na utamaduni wa kiutu na ubinadamu kuishi chini ya himaya ya Bwana Malik na kuchukua mtazamo wa kuridhia kumtumikia kwa uaminifu bwana wao dhalili. Kijakazi alizaliwa na kujikuta katika hali hii ya kutokana na ukoo wa utumwa, akawa mtumwa wa kutumikishwa katika makazi ya Bwana Malik. Mwandishi anatueleza;

Mkewe Bwana Malik, kama alivyo yeye mwenyewe, alipenda sana kumtuma Kijakazi. Kazi za Kijakazi zilikuwa za nenda rudi, mara afanye hili mara afanye lile, mara aende huko mara aende kule, mara achukue hiki mara achukue kile, kutwa kucha. Mara nyingi baada ya kuifanya kazi hurejeshwa kuifanya kazi hiyo hiyo mara ya pili. Kijakazi hakuwa na mapumziko hata kidogo ndani ya nyumba ya Bwana Malik. (uk.1)

Licha ya hali hii, Kijakazi aliamini kuwa ulikuwa wajibu wake kumfurahisha bwana wake kwani hayo ndiyo majaliwa yake. Huo ukawa mwendo wake wa kuridhia kutumika kinyume na haki kwa ajili ya kutimiza matakwa ya bwana wake na kila aliyemhusu. Kijakazi alifikia kujirudi pindi watu wa kasri walipokasirika kwa kosa asilolifanya. Mwandishi anasema,

Hakupenda hata kidogo kumwona yeyote katika watu wa Bwana Malik amekasirika, na ilipokuwa hivyo, alijiona yeye ndiye chanzo na alijilaumu sana. (uk. 1). Hilo halikutosha, pindi Bwana Fuad aliporithi mali ya babake, Bwana Malik, baada ya kufa kwa wazaziwe alimnyanyasa bila huruma. Mwandishi anasema: Fuad

alimnyemelea Kijakazi kidogo kidogo na ilhali yumo usingizini, akampiga teke la ubavu. (uk. 10)

Kijakazi alikuwa amelala bila kukusudia kwa uchovu wa kazi alizokuwa akifanya kama punda. Hata hivyo, Kijakazi hakuona amenyanyashwa bali alijihesabu kama aliyefanya kosa kubwa na kumwomba msamaha Bwana Fuad hali hakufanya kosa lolote. Isitoshe, akatoa ahadi kuwa hatarudia. Utamaduni wake umeyumbishwa kiasi cha kutoona mateso anayopata na kuridhia kuwa hiyo ndiyo hali anayostahiki! Mtazamo wake umefisidika kwa kujiona kuwa hafalii maisha mengine yenye hadhi ila hayo tu: kwamba kama binadamu ana haki ya kupinga maovu na kutokubali kudhulumika. La muhimu kwake ni bwana wake afurahi hata akiwa yeye anadhurika.

Mamwinyi walidhalilisha na kunyanyasa bila hata kujali zuri wanalofanyiwa. Maimuna, mke wa Bwana Malik, alimsukuma Kijakazi akaangukia masufuria akiwa jikoni kwa kuwa amembusu mtoto wao Fuad ilhali yeye mwenyewe Bi. Maimuna alikuwa ameshindwa kumtuliza na kumnyamazisha Fuad pindi anapolia. Huyu Kijakazi ndiye aliyemdaka Fuad pindi mama mtu alipomrusha nusura aanguke chini apasuke kichwa. Hayo yote hayakuwa chochote kwa mamwinyi. Alimnyanyasa na kumtukana kama kiumbe asiye na thamani, “Si huyu mbwa huyu, ati anambusu Fuad” (uk. 4). Hayo yalikuwa maneno ya Bi. Maimuna akimrejelea Kijakazi alipokuwa akimjibu Bwana Malik kufuatia kelele zilizokuwa jikoni wakati alipokuwa akimgombeza Kijakazi kwa kumbusu mwanawe.

Hali hii ya manyanyaso na ukandamizaji haikuwa tu kwa Bwana Malik na baadaye kwa mwanawe Fuad, bali ndiyo iliyokuwa pumzi ya wafanyakazi katika mashamba ya mamwinyi katika kila pembe ya nchi. Hali ilipozidi, walijitokeza kudai haki zao. Hapo ndipo walipokumbana na nguvu za dola ya mkoloni aliyekuwa mshirika na ngao ya mamwinyi. Shafi anasema:

Kila wafanyakazi walipochukua hatua za kudai haki zao waliitwa maaskari wa kikoloni ambao walitumia silaha zao za virungu, mabomu ya kuumiza macho na bunduki kutawanya. Baadhi ya viongozi wao na wafanyakazi wengine jasiri walitiwa vifungoni ambako waliteswa na kufanyiwa ukatili wa kila aina. (uk.11)

Walichotakiwa na mamwinyi na wakoloni ni kubadili utamaduni wao na kuridhia hali hiyo kuwa majaliwa yao. Wao ni watu wa kutumika tu vyovyote vile, si halali yao kuishi maisha ya mabwana zao. Hiyo si hadhi yao. Kwao utiifu ndiyo jambo la msingi na si kulalamika kwamba wanadhulumikiwa au wana haki zao. Wao wasitazamie usawa na mabwana zao. Hali ya kudai haki na kulalamika ni makosa yanayofaa kuadhibiwa vikali. Hata hivyo, joto la dhiki walilopitia wafanyakazi halikuruhusu utamaduni wa kutaka usawa wa kibinadamu na utu kukoma. Mtazamo wao wa kusema haki na kutonyamazia maovu uliendelea chini kwa chini kwa kupanga mikakati ya kujikomboa kutokana na utumwa wa mamwinyi na nguvu za kikoloni. Mwandishi anasema, “...wafanyakazi hawakwisha kufanya migomo, maandamano na mikutano ya hadhara na ya siri kupinga mabepari na makabaila na kudai uhuru kutoka kwa wakoloni.” (uk.11)

Bwana Fuad, hakumstahi au kumjali yeyote katika shamba; kila mtu alikuwa mtu duni wa kutumikishwa tu. Hakumwona yeyote kuwa mtu wa kustahiki ubinadamu. Mwandishi anasema, “Yote haya yalikuwa kwa sababu ya ujeuri, usafihi na utovu wa adabu wa Fuad. Alikuwa hamjali mkubwa au mdogo; kila aliyekuwa akifanya kazi kwake au kwa jumla kila mkulima kwake yeye alikuwa ni mtwana tu” (uk.12)

Mamwinyi kwao ni kawaida kuwanyanyasa wanawake kimapenzi bila kujali. Watakacho wapate kwa hiari au lazima si jambo la kubembeleza. Bwana Fuad alitaka kumbaka Mariam kwa nguvu kwa kushindwa kutaradhia kwa sababu ya ubwana aliokuwa nao. Mariam wakati huo alikuwa katika banda la ng’ombe akifanya kazi zake. Mwandishi anasema, “...mara alimvamia Mariam na kuanza kumbusu mashavuni” (uk.12).

Hapo Mariam alipiga ukulele na kujipapatua kwa nguvu hadi akafaulu na kutoka bandani. Mwandishi anaeleza kuwa tendo hili la kuwanyanyasa kimapenzi wasichana wa wakulima au wafanyakazi wa mabwana shamba lilikuwa jambo la kawaida kwa wana wa mamwinyi. Fuad anafuata tu mkondo wa wenzake naye apate utamu wanaoupata. Anasema, “Mara kwa mara Fuad alisikia hadithi kutoka kwa vijana wenzake, watoto wa mabwana shamba, namna gani watoto wa kike wa kishamba walivyo mahodari katika kuwastarehesha bwana zao” (uk.14)

Haya ndiyo yalikuwa masahibu ya kitumwa ya mabinti wa wakulima, ashakumu si matusi, wakitumiwa kama kopo la chooni na wana wa mabwana shamba kutoa shahawa zao. Hata Mkongwe, mjukuu wa Mzee Sharwani, Fuad alitaka kumbaka pia alipomwingilia kibandani mwake usiku wa manane alipotoka ulevini. “Hakubisha hata hodi alipofika hapo. Aliusukuma mlango wa kumbesa uliokuwa umezuiliwa kwa kisiki cha mti. Mkongwe alishituka na kuruka kutoka pale kitandani alipokuwa amelala akipiga makelele” (uk.30)

Hali ya wakulima ilikuwa mbaya zaidi hasa kutokana na harakati zao za kupinga utawala wa mamwinyi na mabwana shamba. Hapo basi, mabwana shamba walizidisha chuki zao dhidi ya wakulima na kuwafanyia vitendo vingi vya kikatili wakiungwa mkono na wakoloni. Konde zao zilitiwa moto, mazao yao kung’olewa yakiwa machanga na kufukuzwa katika mashamba ya mabwana shamba. Mwandishi anasema : “...Mateso ya mabwana shamba ambao waliungwa mkono na wakoloni yalizidi” (uk. 25)

Yote hiyo ikawa ni jitihada ya kuua kabisa utamaduni wa wakulima wa kutaka kuchukuliwa kama binadamu sawa na mabwana shamba na kuwa na haki ya kupinga maovu na udhalimu dhidi yao na wengineo. Lakini haikuwa rahisi, wakulima walijiunga pamoja kwa unyonge wao kuzinduana na kupanga mkakati mmoja wa kuung’oa utawala wa mamwinyi kote nchini na kuleta mageuzi ya sheria ya umiliki ardhi na falsafa ya kiuchumi itakayojali masilahi ya wote kwa usawa. Kweli kwa juhudi zao licha ya ukatili wa nguvu ya serikali ya kisultani kama asemavyo mwandishi, hatimaye mapinduzi yaliyoongozwa na wakulima na wafanyakazi yalitokea nchini Zanzibar na serikali mpya ya Jamhuri ya Watu wa

Zanzibar iliyoongozwa na Chama cha Afro-Shiraz iliundwa. Hilo likatia kikomo utumwa wa mamwinyi na ukoloni mkongwe ukajigeuza ukoloni mamboleo. Mwandishi anasema : “Serikali ya Ki-Sultani iliyowapa kila haki na uwezo mabwana shamba na mapebari ilipinduliwa...” (uk.53)

Anguko hilo la utawala wa mamwinyi linaleta afueni ya maisha kwa wakulima ambapo sasa wanakatiwa mashamba ya mabwana shamba kuwa miliki yao na kuanzisha kilimo cha ushirika katika sera mpya ya ardhi ambapo ardhi yote ni mali ya serikali. Umari na wakulima wengine wanakatiwa ekari tatu tatu katika shamba la Bwana Fuadi ambaye anatoroka asijulikane alikokwenda kwa kushindwa kuhimili mabadiliko ya sera ya umiliki ardhi na uzalishaji mali iliyoletwa na serikali ya mapinduzi.

4.0 Hitimisho

Makala hii imetumia riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* na diwani ya *Sauti ya Dhiki* kujadili kuhusu mifumo ya utumwa na ukoloni iliyozikabili jamii za Afrika Mashariki na athari zake katika usemi wa utamaduni na mtazamo wa jamii. Ingawa kazi hizi zina umbo tofauti la kifasihi na kukitwa katika masafa tofauti ya kijiografia katika Ukanda wa Afrika Mashariki, zimeonesha ari ya kudumisha fikra za utamaduni na mtazamo wa jamii mbele ya kani ya kuzisambaratisha kwa ukandamizaji kupitia vitisho na nguvu za dola.

Kasri ya Mwinyi Fuad imeonesha nguvu za utumwa na umwinyi uliokitwa katika ukoloni wa Mwingereza ulivyojaribu kwa vitisho na nguvu za dola kuhawilisha utamaduni wa kudumisha haki ya ubinadmu katika mahusiano ya jamii bila kuwachukulia wengine kama nusu-watu na wasio na thamani ya kuishi kama mamwinyi na wenye navyo. Ukipania kuuzika mtazamo wa kutotaka kusaili mambo yanavyokwenda, kutaka kusikilizwa na kupewa hadhi ya kuwa huru kumiliki nyenzo za uzalishaji mali kama wanavyomiliki wakuu wa jamii. Ingawaje utumwa na umwinyi uliyumbisha tamaduni na mtazamo wa wanajamii wengine kama vile wazazi wa Kijakazi, Kijakazi na Mzee Sharwan, bado ulipata nguvu ya kuvuvumka na kujikita katika misimamo ya Mariam, Mkongwe na juhudi za Vuai wakiwemo wakulima wengine. Hatimaye, kukuru kakara ikazaa matunda, utumwa na umwinyi ukabwagwa chini—ikawa afueni ya muda, ukapisha ukoloni mamboleo ambao ulianza kunenepa.

Sauti ya Dhiki imeonesha uovu wa ukoloni kuzika upinzani wa kutaka uhuru kwa mkakati wa tenga—utawale, wakayumba baadhi ya wanajamii kwa kushirikiana na mkoloni kuwakandamiza wengine. Lakini juhudi za kudumisha utamaduni wa kutaka kutendewa haki ya kumiliki nyenzo za kiuchumi na kujitawala zikashamiri kwa Vita vya Maumau hadi ukoloni ukasalimu amri na kuhujuru. Wananchi wakaona afueni na kutarajia uongozi wa haki kutoka kwa ndugu zao waliochukua hatamu za uongozi—kumbe walikuwa wakoloni weusi—wakafakamia mali ya nchi bila ushirika wa ndugu zao. Mauaji, vitisho na dhuluma zikashamiri kwa kila aliyepinga au kukosoa uongozi uliokuwapo. Hilo halikutia kikomo juhudi za kudai

haki kwa uwazi na kwa mafumbo. Ikazuka “Kenya Twendapi?” na kisha *Sauti ya Dhiki* kudumisha utamaduni wa kiutu na kibinadamu. Watu wote wanapaswa kuchukuliwa kuwa na haki ya kufaidi rasilimali ya nchi yao bila ubaguzi ili manufaa yasiwafikie baadhi tu na kuendeleza mtazamo wa kupinga uovu na viongozi waovu. Pia, hii iliwapa indhari kwamba wana mwisho hata kama utakuwa kwa nguvu za Mungu; ikabaki kuwa kesho nzuri ipo, si kama jana.

Katika kazi zote mbili za fasihi, utamaduni wa ubinadamu na utu ndio pumzi za kujenga mustakabali wa jamii yenye heshima na ugavi wa haki na nyenzo za kiuchumi kwa wanajamii; si kwa wachache wenye utajiri wa kuua na kwa upande ule mwingine, wengi wenye umaskini wa kusononesha. Hivyo, kazi hii inachochea tafakuri ya mfumo wa kimaumbile unaojali utu na ubinadamu kikamilifu. Binadamu, pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia aliyofikia, imethibitika kuwa si suala la kinasibu ila ni mpango mahususi wa kimaisha unaoshiria mfumo maalumu wa kuishi.

Marejeleo

- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Allen, J. de V. (2014). *Slaves, Freedmen and the Sultanate of Zanzibar*. London: James Currey.
- Eastman, C. (1994). *Service, Slavery (utumwa) and Swahili Social Reality*. Cologne: University of Cologne.
- Iiffe, J. (1979). *A Modern History of Tanganyika*. London: Cambridge University Press.
- Kimambo, I. N., na Temu, A. J. (1969). *A History of Tanzania*. Nairobi: East African Publishing House.
- Kresse, K. (2016). “Kenya: Twendapi? Re-reading Abdilatif Abdalla’s Pamphlet Fifty Years after Independence.” *Africa*. 86(1):1-32.
- Mwathi, V., Makoti, V., na Mutua, J. (2024). “Mabadiliko ya Utabaka: Ulinganishi wa Riwaya za ‘Kuli’ na ‘Pendo la Karaha’.” *Mwanga wa Lugha* 9(1): 169-175.
- Odetola, T. O na Ademola, A. (1987). *Sociology: An Introductory African Text*. Hong Kong: Macmillan Publishers.
- Shafi, A. (1978). *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.
- Sharma, A., na Gupta, T. (2015). “The Making of Third World: The Impact of Colonization.” *Research Journal of English Language and Literature*, 3(2): 141-144.
- Sheriff, A. (1987). *Slaves, Spices and Ivory in Zanzibar: Integration of an East African Commercial Empire into the World Economy, 1770–1873*. London: James Currey.
- Vierke, C. (2024). “Zanzibari Worlds: A Relational Reading of Abdulrazak Gurnah’s *By the Sea* and Adam Shafi Adam’s *Vuta n’kuvute*.” Katika S.

Moorthy, na A. Jamal (Wah.) *Indian Ocean Studies: Cultural, Social, and Political Perspectives*. Leiden uk. 108 -133.